AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**GERALD KOROSO KALONGE DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI Na. 024/2018**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**TAREHE 13 NOVEMBA 2024**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 13 Novemba 2024**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama), leo, imetoa Hukumu katika kesi ya *Gerald Koroso Kalonge dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Gerald Koroso Kalonge (Mleta Maombi) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi). Wakati wa kuwasilisha Maombi haya, alikuwa amefungwa katika Gereza Kuu la Ruanda, jijini Mbeya, akisubiri kutekelezwa hukumu ya kifo baada ya kupatikana na hatia ya mauaji. Mleta Maombi alidai haki zake zilikiukwa wakati wa kusikiliza kesi yake katika mahakama za ndani ambapo alikutwa na hatia na baadaye kuhukumiwa kifo. Aliomba mahakama ifanye marekebisho, akiomba hatia na hukumu yake vibatilishwe, aachiliwe huru kutoka gerezani, na apewe fidia kwa kuhukumiwa kifo kimakosa.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki), Mahakama iliona kwamba, kwanza ilipaswa kuamua mamlaka yake ya kusikiliza Maombi. Katika suala hili, Mjibu Maombi aliibua pingamizi kuhusu mamlaka ya kisheria ya Mahakama, akidai kwamba Mahakama haikuwa na mamlaka halisi au ya rufaa ya kuingilia kati kuhusu matokeo ya mahakama za ndani. Katika kushughulikia pingamizi hili, Mahakama ilisisitiza msimamo wake kwamba haitumii mamlaka halisi au ya ndani kwenye maamuzi ya mahakama za ndani. Hata hivyo, bado ina mamlaka ya kutathmini endapo kesi za ndani ziliendeshwa kwa namna inayolingana na viwango vilivyowekwa katika vyombo vya kimataifa vya haki za binadamu vilivyoidhinishwa na Serikali husika. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba mamlaka yake ya kisheria yalitimizwa.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Mjibu Maombi, Mahakama ilivichunguza kwa mujibu wa Kanuni zake. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka binafsi kwani, tarehe 29 Machi 2010, Mjibu Maombi iliweka Azimio lililotolewa chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki.

Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430



Azimio hili linaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi dhidi ya Mjibu Maombi kulingana na Kifungu cha 5(3) cha Itifaki. Mahakama ilisisitiza kwamba Mjibu Maombi kuondoa Azimio hilo, mnamo tarehe 21 Novemba 2019, hakukuathiri Maombi haya kwani uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020, wakati Mambi haya yaliwasilisha katika Mahakama mnamo tarehe 28 Septemba 2018.

Kuhusiana na mamlaka ya muda, Mahakama iligundua kuwa madai ya ukiukaji yalitokana na ukweli uliotokea mnamo mwaka 2015, ambapo ni baada ya Mjibu Maombi kuridhia Itifaki na kwa hivyo, Mahakama iliona kuwa ina mamlaka ya muda. Kuhusiana na mamlaka ya kieneo, Mahakama iliona kuwa ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulitokea ndani ya mamlaka ya Mjibu Maombi. Kwa sababu hiyo, Mahakama iliona kuwa ina mamlaka ya kieneo.

Kwa upande wa ukubalifu wa maombi, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 cha Itifaki, Mahakama ililazimika kuamua endapo Maombi haya yalitimiza matakwa ya ukubalifu, kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 56 cha Mkataba na Kanuni ya 50 ya Kanuni za Mahakama (Kanuni). Mahakama kwanza iliangalia pingamizi lililoibuliwa na Mjibu Maombi kuhusu kutokamilisha taratibu zote za ndani. Katika suala hili, iliona kwamba Mleta Maombi alihukumiwa mbele ya Mahakama Kuu ya Tanzania tarehe 30 Juni 2015. Kisha alikata rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa, chombo cha juu cha mahakama katika Serikali ya Mjibu Maombi ambayo ilitupilia mbali rufaa yake mnamo tarehe 12 Oktoba 2017. Kwa hivyo Mahakama ilibainisha kwamba Mleta Maombi alikuwa amekamilisha taratibu za ndani kama inavyotakiwa na Mkataba na Kanuni.

Ingawa masharti mengine ya ukubalifu hayakupingwa na Mjibu Maombi, Mahakama bado ililazimika kujiridhisha kuwa Maombi haya yalizingatia matakwa yote ya ukubalifu kama inavyotakiwa na Kifungu cha 6 cha Itifaki.

Katika suala hili, iliona kwamba, Mleta Maombi walikuwa ametambuliwa dhahiri kwa jina kwa kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama. Iliona pia kwamba madai ya Mleta Maombi yalilenga kulinda haki zake kulingana na Kifungu cha 3(h) cha malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Maombi yalizingatia Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama. Aidha, Mahakama ilibaini kuwa lugha iliyotumiwa katika Maombi haikuwa ya kudharau au kumtukana Mjibu Maombi au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama na pia kwamba Maombi hayakuzingatia tu habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusu ufaafu wa muda wa kuwasilisha Maombi, Mahakama ilibainisha kuwa Maombi haya yaliwasilishwa miezi 11 na siku 16 baada ya kukamilisha taratibu zote za ndani. Kwa kuwa Mleta Maombi

si mwanasheria na aliyefungwa ambaye aliwasilisha Maombi mbele ya Mahakama bila msaada wa wakili, Mahakama ilibainisha kuwa Maombi haya yaliwasilishwa ndani ya muda unaofaa kwa mujibu wa Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama. Mwisho, Mahakama ilibaini kuwa kesi hiyo haikuwa imeshughulikiwa hapo awali mbele ya mahakama nyingine ya kimataifa na kwa hivyo ilizingatia Kanuni ya 50(2)(g) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusu uzingatiaji wa sheria wa kesi hiyo, Mahakama iliangalia endapo Mjibu Maombi alikiuka haki za Mleta Maombi za usawa na ulinzi sawa wa sheria; uhai; utu; kusikilizwa kwa haki; kufurahia maisha ya familia yake na uhuru wa kutembea kama inavyolindwa chini ya Mkataba.

Kuhusu madai ya ukiukaji wa haki ya usawa na ulinzi sawa wa sheria, Mahakama ilibaini kwamba Mleta Maombi hakuwa amethibitisha madai hayo na, kwa hivyo, ilibaini kwamba Mjibu Maombi hakuwa amekiuka Kifungu cha 3 cha Mkataba.

Kuhusu madai ya ukiukaji wa haki ya kuishi chini ya Kifungu cha 4 cha Mkataba, Mahakama ilibainisha, katika nchi ya Mjibu Maombi, adhabu ya kifo ilitolewa na Kanuni ya Adhabu na ilitimizwa na Mahakama Kuu, ambayo ilikuwa mahakama yenye sifa stahiki. Kuhusu endapo ilitimizwa kwa kufuata mchakato unaostahili, ingawa, Mahakama haikuona kosa lolote katika mchakato wa kusikiliza kesi uliosababisha Mleta Maombi kuwekwa hatiani, ilibainisha kwamba adhabu ya kifo ilitumika kwa lazima na hivyo kumfanya jaji asitumie busara ya mahakama kutoa hukumu. Mahakama ilibainisha kuwa jambo hilo lilikuwa ni ukiukaji wa kanuni ya mchakato unaostahili. Kwa sababu ya ukiukaji wa mchakato unaostahili ambao unasababisha adhabu ya kifo ya lazima, Mahakama iliona kwamba Mjibu Maombi alikuwa amekiuka haki ya kuishi chini ya Kifungu cha 4 cha Mkataba.

Mahakama pia iliamua kwamba haki ya utu ya Mleta Maombi chini ya Kifungu cha 5 cha Mkataba ilikuwa imekiukwa kwa sababu ya kuhukumiwa kifo kwa kunyongwa kwa sababu kunyongwa kwa asili ni kudhalilisha na kunapoteza utu wa mtu.

Kuhusiana na madai ya ukiukaji wa haki ya kusikilizwa kwa haki chini ya Kifungu cha 7 cha Mkataba, baada ya kutathmini madai ya Mleta Maombi kuhusiana na ukosefu wa ushahidi wa kutosha ambao ulisababisha hukumu yake; mahakama za ndani kutegemea ushahidi wa vinasaba (DNA); na kuachiliwa huru kwa wakata rufaa weza wa Mleta Maombi, Mahakama haikuona chochote cha kulaumu njia iliyochukuliwa na mahakama za ndani. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Mjibu Maombi hakukiuka haki ya Mleta Maombi ya kusikilizwa kwa haki.

Mahakama pia ilibaini kwamba haki ya Mleta Maombi ya maisha ya familia chini ya Kifungu cha 18 cha Mkataba, na haki ya uhuru wa kutembea chini ya Kifungu cha 12 cha Mkataba hazikukiukwa, kwani madai hayo yalitokana na hatia na hukumu ya Mleta Maombi ambayo Mahakama haikuona kuna makosa.

Mahakama baada ya kubainisha ukiukaji wa Kifungu cha 4 na 5 cha Mkataba kuhusu adhabu ya kifo ya lazima na utekelezaji wa hukumu ya kifo kwa kunyongwa, iliamuru Mjibu Maombi amlipe Mleta Maombi fidia ya kiasi cha Shilingi Laki Tatu (TZS 300,000) kama fidia ya hasara ya kimaadili. Mahakama pia iliamuru Mjibu Maombi, ndani ya miezi sita, aondoe adhabu ya kifo ya lazima kwenye sheria zake na afute kunyongwa kama njia ya kutekeleza adhabu ya kifo. Mahakama pia iliamuru Mjibu Maombi, ndani ya mwaka mmoja, amwondoe Mleta Maombi kwenye adhabu ya kifo na asikilize tena kesi yake kuhusu hukumu kulingana na utaratibu ambao unaruhusu busara ya mahakama.

Hata hivyo, Mahakama ilikataa ombi la Mleta Maombi la kufuta hatia yake, ikibaini kwamba haikuona Mleta Maombi alitiwa hatiani kinyume cha sheria. Kuhusu maombi ya kuachiliwa huru, Mahakama iliona kwamba Mleta Maombi alishindwa kuonyesha hali maalumu ambazo zinalazimisha kuhalalisha kuachiliwa kwake na kwa hivyo ilitupilia mbali ombi hili.

Pia Mahakama iliamuru kwamba hukumu hii ichapishwe ndani ya miezi mitatu, kwenye tovuti za Mahakama ya Mjibu Maombi, na Wizara ya Katiba na Sheria na Mjibu Maombi aripoti kuhusu utekelezaji wa hukumu ndani ya miezi sita baada ya kupokea taarifa.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 70(3) ya Kanuni za Mahakama, Jaji Blaise Tchikaya na Jaji Dumisa B. Ntsebeza walitoa Maazimio kuhusu suala la adhabu ya kifo.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, inaweza kupatikana kwenye tovuti kwenye: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/024/2018.

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa.*

*Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*